



**TAARIFA FUPI YA MTENDAJI MKUU WA SHIRIKA LA RELI TANZANIA NDG.
MASANJA KADOGOSA KWA MH. WAZIRI MKUU JUU YA MAENDELEO YA MRADI
WA UJENZI WA RELI YA KISASA (STANDARD GAUGE) AWAMU YA KWANZA KATI
YA DAR ES SALAAM NA MWANZA TAREHE 28 OKTOBA, 2018:**

1. Utangulizi

Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Nd. Kassim Majaliwa, Waheshimiwa Wageni wote ITIFAKI imezingatiwa.

Mh. Waziri Mkuu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Shirika la Reli (TRC), imeanza utekelezaji wa ujenzi wa mfumo wa reli mpya ya kisasa yaani "Standard Gauge Railway - (SGR)", awamu ya kwanza katika ya DAR-MZA yenye km 1,219 kwa njia kuu iliyogawanywa katika vipande 5 kama ifuatavyo.

| Na. | Kipande | Jumla (km) | Njia kuu (km) | Kupishana (Km) |
|------------|-------------------------|-------------------|----------------------|-----------------------|
| 1. | Dar es salaam- Morogoro | 300 | 205 | 95 |
| 2. | Morogoro -Makutupora | 422 | 336 | 86 |
| 3. | Makutupora-Tabora | 376.5 | 294 | 73.5 |
| 4. | Tabora-Isaka | 162.5 | 130 | 32.5 |
| 5. | Isaka mwanza | 311.25 | 249 | 62.5 |

Reli hii ya SGR ikikamilika itachochea mipango ya Serikali ya awamu ya tano katika kutekeleza sera ya Viwanda na kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa katika ifikapo mwaka 2025. Aidha reli hii itachochea mapinduzi ya kiuchumi kwa kanda nzima ya Afrika Mashariki na Katu hususani Nchi zisizopakana na Bahari.

2. Muda wa Mradi

Kwa mujibu wa mpango kazi mradi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora (Singida) unatazamiwa uwe umekamilika ifikapo Februari 2021. Kipande cha kwanza katika ya Dar es salaam na Morogoro kilisainiwa tarehe 3 Februari 2017, ujenzi ulianza tarehe 2 Mei 2017 na kitakamilika ifikapo 2 Novemba 2019 na kipande cha Morogoro -Makutupora mkataba wake ulisainiwa tarehe 29 Septemba 2017 na ujenzi kuanza tarehe 26 Februari 2018 na kitakamilika tarehe 25 Februari 2021.

3. Wakandarasi wa Mradi

Jumla ya Kilomita 722 za ujenzi wa reli kwa sasa zinatekelezwa katika vipande 2.kipande cha Dar es Salaam-Morogoro kilomita 300 kinajengwa na ubia wa kampuni ya YAPI MERKEZI ya Uturuki na MOTA- ENGIL ya Ureno na kipande cha Morogoro Makutupora chenye kilomita 422 kinajengwa na Kampuni ya YAPI MERKEZI.

4. Wasimamizi wa Mradi

Mhandisi Mshauri (yaani Consultant) anayesimamia mradi huu kwa niaba ya Serikali ni Kampuni ya KORAIL JV ambayo ni ubia wa Kampuni nane za KORAIL, CHEIL na DMEC kutoka Korea, MULTTECH kutoka Botswana, kampuni ya kizawa ya UNITEC kutoka Tanzania, BARAJI kutoka India, SSF kutoka Ujerumani na RINA kutoka Italia

5. Gharama ya Mradi

Kwa kipande cha Dar es Salaam-Morogoro ni Shilingi za Kitanzania Trilioni 2.7 na kwa Kipande cha Morogoro Makutupora ni kiasi cha shilingi za Kitanzania Trilioni 4.4, Jumla ya fedha zote kwenye ujenzi huu ni shilingi Trilioni 7.1 ambazo ni pesa za walipa Kodi wa Tanzania.

6. Mchanganuo wa Shughuli Muhimu za Mradi zinazoendelea

Mh. Waziri Mkuu, ufuatao ni mchanganuo kwa ufupi wa shughuli muhimu zinazoendelea ndani ya mradi wa SGR:

- **Ukataji Milima na Ujazaji wa mabonde (Earthworks)**

Kuna Jumla ya mita za ujazo milioni 23.4 za kifusi zitakazokatwa na kujazwa katika kipande cha kwanza ambapo mpaka sasa zimefanyika mita za ujazo milioni 12.7 sawa na asilimia 55.

- **Ujenzi wa Madaraja**

Kazi ya ujenzi wa madaraja na makalavati unaendelea ambapo daraja refu katikati ya jiji la Dar es salaam lina jumla ya Kilomita 2.56 na ujenzi wake umefikia asilimia 46. Kuna Madaraja ya kati 26 na Makalavati 243, Madaraja ya Treni kupita juu 17, Madaraja ya treni kupita chini 15 na Madaraja ya reli juu ya reli (rail over rail) 5.

- **Ujenzi wa Stesheni**

Jumla ya stesheni 6 zitajengwa kati ya Dar es salaam na Morogoro, kati ya hizo stesheni kubwa ni mbili na stesheni ni ndogo ni 4. Usanifu wa Stesheni hizi umezingatia mazingira na asili ya Tanzania ambapo stesheni ya Dar es Salaam ina sura ya madini adimu ya Tanzanite wakati stesheni za kati usanifu wake umezingatia utamaduni na nyumba zetu za asili. Stesheni ya Morogoro itaonesha uhalisia wa milima ya Uruguru.

- **Mfumo wa uendeshaji Treni (Electrification line)**

Katika mradi huu treni zitaendeshwa kwa kutumia nishati ya umeme kutoka Tanesco na tayari taratibu za kumpata mkandarasi wa kujenga njia za umeme upo katika hatua za mwisho.

- **Mfumo wa Mawasiliano (Telecommunication& Signalling)**

Mfumo wa Kisasa zaidi uitwao kwa kitaalamu European Train Control System Level 2 utatumika na kuongeza ufanisi wa uendeshaji na usalama wa treni ambapo treni zitaongozwa kuitia kituo maalum (Central Train Control).

- **Karakana Kuu na Kituo cha kuunganishia mabehewa.**

Kutakuwa na karakana kubwa na Kituo kikuu cha kuunganishia treni zenyetunza urefu wa kilometra mbili kinachojengwa katika eneo la Kwala wilayani Kibaha.

Lengo la kituo hiki ni kuunganisha shughuli za reli na bandari kavu (ICD) iliyoko eneo hilo na kupunguza msongamano wa magari makubwa yaingiayo na kutoka jijini Dar es salaam.

Aidha kituo hiki kitaongeza ufanisi wa kuingiza na kuondoa mizigo katika bandari ya Dar es salaam ambapo mizigo itachukuliwa na treni fupi fupi ambazo zitaunganishwa hadi kuwa na urefu wa kilomita 2 katika kituo hiki cha Kwala kabla ya kuendelea na safari zake kuelekea mikoani na nchi jirani.

- **Utandikaji wa Reli**

Mh. Waziri Mkuu, utandikaji wa reli umeshaanza ambapo mpaka sasa jumla ya Kilomita 10 zimetandikwa. Tani 7,250 za reli sawa na urefu wa kilometra 60 zimeshapokelewa na zinaendelea kutumika katika utandikaji huo. Pia mnamo tarehe 23.10.2018 zimepokelewa meli mbili bandarini zenyetunza jumla ya tani 6,500 za reli sawa na urefu wa kilometra 54 na hivyo kufanya jumla ya reli zilizopokelewa kuwa tani 13,750 sawa na urefu wa kilometra 114.

Mataruma yatakayotumika katika mradi huu ni 500,100 kwa kipande cha Dar es salaam – Morogoro wakati kwa kipande cha Morogoro – Makutupora yatahitajika mataruma 703,300. Mataruma yote haya yanatengenezwa hapa nchini katika eneo la mradi.

Hadi sasa kiwanda cha mataruma haya kilichoko Soga - Kibaha kimeshazalisha mataruma 27,000 ambayo ni sawa na asilimia 5.4%.

Mh. Waziri Mkuu, Kulingana na Mkataba wa kipande cha Dar es Salaam Morogoro,mara baada ya kuzalisha mataruma ya ujenzi wa reli wa Kilomita 500, kiwanda hiki kitarudi kuwa mali ya Serikali na hivyo kuongeza idadi ya viwanda nchini.

- **Ajira**

Jumla ya wafanyakazi 5,440, vibarua ni 4,743 ambayo asilimia 96% ni watanzania na 4% ni wageni, wataalamu 189 wa kitanzania na 258 wa kigeni kwa uwiano wa 42% watanzania na 58% wageni. Hata hivyo,Mkataba ulimtaka mkandarasi kuwa na uwiano wa 20% watanzania na 80% wageni kwenye kada ya wataalamu ambapo mpaka sasa amevuka kiwango hicho kwa kuwashirikisha watalamu wengi wa kitanzania moja kwa moja.

Kwa upande wa wafanyakazi wasio na utaalamu (semi-skilled) kimkataba uwiano ulikuwa 80% watanzania na 20% wageni lakini mpaka sasa mkandarasi amevuka uwiano huo kwa kuwashirikisha watanzania kwa asilimia 96%

Pia jumla ya ajira 626 za watanzania wasio na utaalamu na 19 za wenye utaalamu zimepatikana kuititia kampuni za wazawa (Sub-Contractors) wanaoshiriki moja kwa moja kwenye mradi huu.

- **Wananchi walioathiriwa na Mradi**

Ardhi na mali nyingine za wananchi wapatao 6,514 zenyetunza thamani kiasi cha shilingi za kitanzania billion 83.099 zitatakiwa kuhamishwa ili kupisha ujenzi wa Reli kwa kipande cha Dar es Salaam-Morogoro.

7. Kazi zinazoendelea Kipande cha Morogoro-Makutupora

Mh. Waziri Mkuu, zifuatazo ni shughuli zinazoendelea kwa kipande cha Morogoro - Makutupora

- **Maandalizi (Mobilization)**

Kazi zinazoendelea ni Ujenzi wa kambi za Kilosa na Ihumwa, maandalizi ya vifaa vya ujenzi, mitambo na wataalamu.

- **Uthamini wa ardhi**

Uthamini wa ardhi itakayochukuliwa unaendelea ambapo jumla ya kilometra 116 zimekamilika katika meneo ya Morogoro – Kilosa na Ihumwa (Dodoma) hadi Gulwe (Mpwapwa) na kazi hiyo inaendelea.

- **Utafiti Wa Ubora Wa Udongo na miamba kwa ajili Ujenzi wa Tuta Na Misingi Ya Madaraja unaendelea**

- **Ujenzi wa tuta:**

Ujenzi wa tuta umeanza ambapo jumla ya kilometra 80 zimesafishwa na kazi ya kukata na kujaza udongo imefikia urefu wa kilometra 33.

- **Udhibiti wa athari za kiafya, kijamii, usalama na mazingira (Health, Safety and Environment (HSSE))**

Mh. Waziri Mkuu, **kwa ujumla maendeleo ya mradi ni 32% kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro na 3.31% kwa kipande cha Morogoro -Makutupora ni**

FAIDA ZA MRADI

Mheshimiwa Waziri Mkuii, faida ya mradi huu imegawanyika katika sehemu zifuatazo:

1. Wakati wa Ujenzi

- Mradi mpaka sasa umetoa ajira zipatazo 5,440 za moja kwa moja na umechangia kutoa ajira na kukuza vipato vya wananchi wanaouzunguka ambao wanashiriki katika kutoa huduma mbali mbali katika mradi huu.
- Kuchangia katika pato la taifa na sera ya viwanda: mradi huu umeongeza mahitaji makubwa ya cement, Kokoto, nondo pamoja na vifaa vingine vya ujenzi hivyo kuvifanya viwanda vyetu vya ndani kupata soko la bidhaa zake.
- Katika kuitia ongezeko la mahitaji ya vifaa vya ujenzi ajira nyingine zimezalishwa kwenye viwanda hivo.
- Sekta ya usafirishaji pia imefaidika kwani kuna baadhi ya watanzania wamekodisha magari yao pamoja na kushiriki moja kwa moja katika usafirishaji wa vifaa na mitambo mbalimbali
- Baadhi ya wakandarasi wazawa wanashiriki moja kwa moja kutoa huduma za kandarasi (sub-contracts) za ujenzi.

2. Wakati wa uendeshaji

Mh. Waziri Mkuu, Mradi utakapokamilika utakuwa na faida zifuatazo:

- Kuongeza ufanisi wa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kupunguza muda wa safari mathalani Dar es salaam-Morogoro safari kuwa saa 1 na dk 15, safari ya DSM – Dodoma muda wa safari utakuwa masaa 3.
- Kupunguza gharama za usafirishaji mizigo, inategewa mara mradi utakapoanza gharama za usafirishaji wa mizigo itashuka kwa asilimia 40% na kuifanya bandari ya Dar es salaam kuhimili ushindani.
- Kuchocha uanzishwaji wa viwanda maeneo mengine ya nchi na kutoa uhakika wa usafirishaji wa mali ghafi na bidhaa.
- Mradi utachocha uanzishwaji wa miji midogo katika sehemu zinazojengwa stesheni ambazo zitakuwa kivutio kwa wananchi, mfano maeneo ya Soga, Ruvu na Kwala kwa Mkoa wa Pwani.

3. Mapendekezo kwa Sekta zingine

- Kwa maeneo kama ya stesheni za Soga, Ruvu na Kwala, yaliyo Mkoa wa Pwani tunashauri uwepo mkakati wa kupanga miji midogo kwa kupima ardhi.
- Kwa eneo la Kwala ambalo litajengwa Kituo kikubwa cha mizigo na karakana za ukarabati wa matreni, mkabala na bandari kavu inapendekezwa kuanzishwe ukanda wa viwanda (industrial Zone) ili kuvutia wawekezaji kuwekeza sehemu ambayo malighafi na bidhaa zao zitasafirishwa kutoka na kuingia kwenye viwanda vyao.

HITIMISHO

Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kuipongeza Serikali ya Awamu ya tano (5) chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais daktari. John Pombe Joseph Magufuli kwa uthubutu wa kuanzisha ujenzi wa reli hii ya kisasa.

Reli hii ni mhimili mkubwa na thabit katika ukuaji wa uchumi wa Taifa. Mapinduzi ya Sekta za viwanda, kilimo, Ujenzi, ufugaji, usafirishaji, madini pamoja na Utalii yatachagizwa na uwekezaji huu mkubwa.

Nawasilisha.

Masanja K. Kadogosa

MKURUGENZI MKUU